



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**



**TAARIFA KWA UMMA**

**KUHUSU RATIBA YA UCHAGUZI MDOGO WA**

**UDIWANI KATIKA KATA 32 ZA TANZANIA BARA**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi imepokea taarifa kutoka kwa Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa ambaye kwa kutumia mamlaka aliyopewa chini ya Kifungu cha 13(1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa Sura ya 292 R.E.2015, akiitaarifu Tume uwepo wa nafasi wazi za Madiwani katika Kata 31 za Tanzania Bara. Nafasi hizo wazi zimetokana na sababu mbalimbali ikiwemo vifo na kujiuzulu.

Aidha, Tume inatangaza kufanyika kwa Uchaguzi Mdogo wa Udiwani katika Kata ya Kitangiri Halmashauri ya Wilaya ya Ilemela sambamba na Kata hizo 31. Uchaguzi katika Kata ya Kitangiri utafanyika baada ya Mahakama ya Rufaa kuondoa maombi ya mapitio yaliyowasilishwa katika Mahakama hiyo kufuatia kutenguliwa kwa matokeo ya Uchaguzi wa Udiwani katika Kata hiyo.

Kwa kuzingatia matakwa ya kifungu cha 13(3) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatoa taarifa kwa Umma kuhusu uwepo wa Uchaguzi mdogo wa Udiwani katika Kata Thelathini na Mbili (32) zilizopo katika Halmashauri Ishirini (20) za Tanzania Bara.

Tume imepanga kuendesha Uchaguzi mdogo katika Kata hizo 32 kwa kuzingatia Ratiba ifuatayo:

1. Fomu za Uteuzi wa Wagombea zitatolewa kati ya tarehe 27 hadi 31 mwezi Mei mwaka huu.
2. Uteuzi wa Wagombea utafanyika tarehe 31 mwezi Mei mwaka huu
3. Kampeni za Uchaguzi zitafanyika kuanzia tarehe 01 mwezi Juni hadi tarehe 14 mwezi Juni mwaka huu na
4. Siku ya Uchaguzi itakuwa ni tarehe 15 Mwezi Juni mwaka huu

Tunapenda kuvikumbusha Vyama vya Siasa na wadau wote wa Uchaguzi kuzingatia Sheria, Kanuni, Maadili ya Uchaguzi, Taratibu, Miongozo na maelekezo yanayotolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi wakati wa kipindi chote cha Uchaguzi huu mdogo.

Imetolewa leo tarehe 21 Mei, mwaka huu.

Jaji (R) Mbarouk S. Mbarouk  
**MAKAMU MWENYEKITI**  
**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**

## KATA ZILIZOWAZI

NA	MKOA	NA	HALMASHAURI	NA	KATA
1.	ARUSHA	1	Halmashauri ya Wilaya ya Monduli	1	Mto wa Mbu
				2	Mkuyuni
				3	Majengo
		2	Halmashauri ya Wilaya ya Karatu	4	Ganako
				5	Daa
				6	Mbulumbu
				7	Oldeani
				8	Kanssay
2.	RUVUMA	3	Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo	9	Likuyuseka
3	DODOMA	4	Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa	10	Kinyasiti kati
		5	Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma	11	Kikombo
4	KATAVI	6	Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo	12	Itenka
5	TABORA	7	Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge	13	Ipole
				14	Pangale
		8	Halmashauri ya Wilaya ya Igunga	15	Itumba
6	IRINGA	9	Halmashauri ya Mji wa Mafinga	16	Boma
7	MTWARA	10	Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani	17	Tandika
				18	Chikongola
8	DARES SALAAM	11	Halmashauri ya Manispaa ya Ilala	19	Bonyokwa
		12	Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni	20	Tungi

NA	MKOA	NA	HALMASHAURI	NA	KATA
		13	Halmashauri ya Manispaa ya Temeke	21	Chang'ombe
9	LINDI	14	Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa	22	Ruangwa
10	SIMIYU	15	Halmashauri ya Wilaya ya Busega	23	Mkula
				24	Lamadi
11	KILIMANJARO	16	Halmashauri ya Wilaya ya Moshi	25	Kibosho Magharibi
				26	Uru Shimbwe
12	MARA	17	Halmashauri ya Wilaya ya Musoma	27	Murangi
13	SINGIDA	18	Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi	28	Siuyu
14	KAGERA	19	Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba	29	Kyaitoke
				30	Mugajale
				31	Ruhunga
15	MWANZA	20	Halmashauri ya Wilaya ya Ilemela	32	Kitangiri